UNECE

Azimio la Ukuzaji wa Usawa wa Kijinsia Kwenye Viwango na Mashirika Ya Viwango

UNITED NATIONS

UNECE

Azimio la Ukuzaji wa Usawa wa Kijinsia Kwenye Viwango na Mashirika Ya Viwango

Excerpt of Document:
Revised Recommendation U
on Gender Responsive Standards
(ECE/CTCS/WP.6/2018/6/Rev.1)

UNITED NATIONS

Note

The designations employed and the presentation of material in this publication do not imply the expression of any opinion whatsoever on the part of the Secretariat of the United Nations concerning the legal status of any country, territory, city or area, or of its authorities, or concerning the delimitations of its frontiers or boundaries.

Utangulizi

Anzilishi kuu la Viwango na Usawa wa Kijinsia ya UNECE ni kikundi la wataalamu walioapishwa na uamuzi wa kamati za serikali mbali mbali, lina mipango ya kueneza umuhimu wa usawa wa kijinsia katika ukuzaji, utumiaji, na athari za viwango kwenye mashirika. Kikundi hiki kilianzishwa mnamo mwaka 2016 na nia zifuatazo: (i) kuimarisha matumizi ya viwango ili kutimiza SDG 5 (Kufikia usawa wa kijinsia na kuwezesha Wanawake na Wasichana); (ii) kueneza usawa wa kijinsia katika uundaji na maendeleo ya viwango na sera mbalimbali; (iii) kufafanua viashiria vya jinsia na vigezo vinavyoweza kutumika katika maendeleo ya viwango.

Ili kufikia malengo haya, anzilishi hili limeleta pamoja wataalamu kutoka mashirika kadhaa ya viwango, pamoja na: wataalamu wanaohusika na masuala ya kijinsia na uwezeshaji wa wanawake, wawakilishi wa miili ya udhibiti na watunga sera, NGOs, Mashirika ya Umoja wa Mataifa na wajumbe wa kimataifa. Mikutano inaruhusu washiriki kubadilishana maarifa na maripoti juu ya mafanikio ya kufikia usawa wa kijinsia katika viwango na mashirika ya viwango.

Ujumuishi wa usawa wa kijinsia katika viwango na mashirika ya viwango utadumisha maendeleo ya kiuchumi na pia kupunguza ubaguzi wa usawa. Aidha, viwango vya kukabiliana na kijinsia vitasaidia kuhakikisha mazingira ya kazi salama kwa wafanyakazi wote.

Anzilishi hili linaungwa mkono na Shiriki la Umoja wa Mataifa ya bara Uropa (UNECE), jukwaa la ushirikiano kati ya jamii na viongozi wa viwango shirika la sita (W.P.6): UNECE, WP.6, (i) hustawisha matumizi ya viwango na watunga sera na biashara kama chombo cha kupunguza vikwazo vya biashara; (ii) inahimiza uwezo wa kukabiliana na maafa, innovation na utawala bora; na (iii) inatetea matumizi ya viwango katika utekelezaji wa malengo ya Umoja wa Mataifa, pamoja na utekelezaji wa Ajenda 2030 na Mfumo wa Sendai wa Kupunguza Hatari za Maafa.

.

.

Azimio

Ushirikiano:

Sisi kama shiriki kuu la kitaifa ya viwango/ shiriki la viwango:

- Tunakiri mradi wa tano kulingana na Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa inayotendekeza usawa wa kijinsia hususa wanawake na wasichana ambao wanakabiliwa na vikwazo vinavyowazuia kufikia uwezo wao kamili;

- Tunakiri umuhimu na ushawishi wa viwango katika majamii mbali mbali;

- Tunakiri ya kwamba uwakilishi wa wanawake katika mashirika ya viwango iko chini ya usawa, na pia matokeo ya viwango baina ya wanawake na wanaume hayatiwi maanani katika harakati za ukuzaji;

- Tunafahamu ya kwamba ni muhimu kuhusisha wanawake katika ukuzaji wa maudhui ya viwango kwani ni fursa ya kutekeleza usawa wa kijinsia;

- Tunafahamu ya kuwa mashirika ya viwango vya kitaifa na vinginevyo, yana miradi tofauti kulingana mujibu wao na miundombinu yaliyoimarishwa;

- Tunaimisha ya kwamba tutajitahidi ili kutimiza:
    - Mashirika ya Viwango yaliyo na usawa wa kijinsia;
    - Viwango vya usawa wa kijinsia;
    - Usawa ndani ya viwango vyote katika miundombinu ya mashirika ya viwango; (pia ya kitaifa na kilimwengu);
    - Kuboresha ujuzi wa ukuzaji wa viwango vya usawa;

Kwa hivyo, tunaahidi ya kuwa, viwango na mbinu za ukuzaji wa viwango yatatathmini usawa wa kijinsia kupitia:

1. Uthibitishi wa Azimio la Ukuzaji wa Usawa wa Kijinsia kwenye Viwango na Mashirika ya Viwango

2. Uzuaji na utekelezaji wa mikakati ya kuboresha usawa wa kijinsia katika shirika letu

3. Ufuatiliaji wa maendeleo; kukusanya na kueneza data, masimulizi na mafanikio makuu.

Sahihi iliyoidhinishwa:

Nota Bene:

Sehemu kiambatisho ambayo imehifadhiwa na UNECE katika tovuti ya UNECE, inataja maelezo na vitendo ambayo mashirika ya viwango yanaweza kuhifadhi katika mikakati ya kuboresha na kueneza usawa wa kijinsia katika viwango na mashirika ya viwango.

Ni juhudi la kila shirika kuamuru mipango ya kuzingatia usawa wa kijinsia. Orodha ya maelezo na vitendo hayajatajwa kina kusudi ya kuwezesha uhuru katika ukuzaji na utekelezaji wa hatua za usawa wa kijinsia ndani ya mashirika ya viwango.

Sehemu Kiambatisho
Azimio la Ukuzaji wa Usawa wa Kijinsia Kwenye Viwango na Mashirika ya Viwango

Utangulizi

Sehemu kiambatisho ambayo imehifadhiwa na UNECE katika tovuti ya UNECE, inataja maelezo na vitendo ambayo mashirika ya viwango yanaweza kuhifadhi katika mikakati ya kuboresha na kueneza usawa wa kijinsia katika viwango na mashirika ya viwango.

Ni juhudi la kila shirika kuamuru mipango ya kuzingatia usawa wa kijinsia. Orodha ya maelezo na vitendo hayajatajwa kina kusudi ya kuwezesha uhuru katika ukuzaji na utekelezaji wa hatua za usawa wa kijinsia ndani ya mashirika ya viwango.

Kiambatisho

Orodha ya Hatua n.1: Kuwezesha Usawa wa Kijinsia katika ukuzaji wa Viwango kwenye mashirika au maeneo mbali mbali

- ❖ Kutahidi usawa baina ya wajumbe wakiume na wakika katika awamu za ukuzaji wa Viwango
    - ➢ Kukadiri usawa wa kijinsia katika baraza mbali mbali na kutambulisha maeneo yanayohitaji maendeleo;
    - ➢ Ungana na mashirika kadha wa kadha ili kuboresha usawa wa kijinsia kwenye kamati zetu za istlahi;
    - ➢ Kusanya data za kijinsia kwa wale wanahusika na ukuzaji wa viwango na kuzilinganisha na takwimu za ajira;
        - ▪ Kwa Mfano: uchoraji wa jedwali ambalo litaonyesha usawa wa kijinsia kwenye kamati za istlahi, sasisha kila mwaka kulingana na viwanda;
- ❖ Kutahidi ukuzaji wa maeneo ya viwango kuwa na usawa jumuisho wa kijinsia
    - ➢ Hakikisha ya kwamba uongozi unaambatana na uboreshaji wa usawa wa kijinsia kwenye mashirika ya viwango;
    - ➢ Fanya utafiti kila mwaka pamoja na kamati kadha wa kadha ili kueleimishana kuhusu usawa wa kijinsia;
    - ➢ Kuza na tekeleza sera, shughuli ambazo zinahimili usawa wa kijinsia (kwa mfano; kuhamasisha na kuelemisha wale ambao wako kwenye kamati za ukuzaji wa viwango);
    - ➢ Tathmini usawa wa kijinsia kwenye viti vya uongozi ili kutambua maeneo yanayohitaji kuboreshwa ili kuambatana na usawa wa kijinsia;
- ❖ Unga mkono wale ambao wangependa kusimamia usawa wa kijinsia katika viwanda vya ukuzaji wa viwango;
    - ➢ Himiza viongozi na wasimamizi kustawisha usawa wa kijinsia katika kamati za ukuzaji wa viwango kwa kuwapa rasilimali ambazo wanahitaji;
    - ➢ Eneza matukio, ripoti, maarifa kuhusu usawa wa kijinsia kwa mashirika ya ukuzaji wa viwango;
- ❖ Kutahidi usawa katika ushirikishwaji wa ukuzaji wa viwango kwa njia ya kuandika vidokezo;
- ❖ Hakikisha ya kua orodha ya usawa wa kijinsia inaambatana na malengo ya usawa wa kijinsia ili kuwezesha ufuatiliaji;

Orodha ya hatua n.2: Kuwezesha viwango vya usawa wa kijinsia

- ❖ Kutahidi upekuaji wa wataalamu ambao watawezesha ukuzaji wa viwango vya usawa wa kijinsia;

- ❖ Changia katika ukuzaji wa mbinu ambazo zitasaidia kuchambua usawa wa kijinsia katika mashirikia ya viwango ili kusisitiza na kuhakikisha ya kwamba viwango ni vya usawa wa kijinsia. Kwa Mfano GBA+

- ❖ Toa fursa ya mafunzo hususa zana za kuwezesha usawa wa kijinsia katika viwango ili kukadiri kamili matokeo;

- ❖ Tumia sera zilizomo (kwa mfano. ISO, CEN-CENELEC, ITU, IEC na kadhalika) ili kuwezesha uboreshaji wa utaalamu;

- ❖ Hakikisha kamati zina rasilimali, taalamu ili kukuza viwango vya usawa wa kijinsia kwa; za kutosha

  - ➢ Kuandaa mafunzo yoyote muhimu ya kuendeleza ujuzi wa kamati kuhusu usawa wa kijinsia;

  - ➢ Kuhakikikisha uhusishaji wa mtaalam wa usawa wa kijinsia (kwa mafano kupitia mtandao wa wataalam wa kijinsia)

- ❖ Kutahidi urasimishaji wa mafanikio ya sera ili kuhakikisha uendelezaji wa usawa wa kijinsia kwenye viwango;

Orodha ya Hatua n. 3: Kuwezesha mashirika ya viwango vya usawa wa kijinsia

- ❖ Tathmini, endeleza au pokea taalamu zinahitajika ili kuwezesha utelekesaji wa usawa wa kijinsia;

- ❖ Kusanya data ya uwiano wa kijinsia ya wanaibu katika mashirika ya viwango;

- ❖ Endeleza zana za mafunzo ili kuboresha utambuzi wa usawa wa kijinsia wa wafanyakazi;

- ❖ Fuatilia na rekodi ushirikishi na matokeo ya mafunzo yaliyotimizwa.

Azimio la Ukuzaji wa Usawa wa Kijinsia Kwenye Viwango na Mashirika Ya Viwango

United Nations Economic Commission for Europe

Palais des Nations
CH - 1211 Geneva 10, Switzerland
Telephone: +41 22 917 44 44
E-mail: regulatory.cooperation@un.org
Website: http://www.unece.org

Excerpt of Document: Revised Recommendation U on Gender Responsive Standards (ECE/CTCS/WP.6/2018/6/Rev.1)